ARTICLE 19

GLOBAL CAMPAIGN FOR FREE EXPRESSION

Kanuni za Camden za Uhuru wa Kujieleza na Usawa

Juni 2010

ARTICLE 19
GLOBAL CAMPAIGN FOR FREE EXPRESSION

ARTICLE 19
Free World Centre
60 Farrington Road
London
EC1R 3GA
UINGEREZA

Simu: +44 20 7324 2500
Kipepesi: +44 20 7490 0566
Barua Pepe: info@article 19.org

© ARTICLE 19, London
ISBN 978-1-906586-18-8

ARTICLE 19 Kenya & Eastern Africa
ACS Plaza, 3rd Floor
Lenana Road, Kilimani
Sanduku la Posta 2653,00100
Nairobi, Kenya
Simu: +254 20 3862230/2
Kipepesi:+254 20 3862231

ARTICLE 19 inahimiza mashirika na watu binafsi kuidhinisha Kanuni za Camden. Pia tunahimiza mtupe maoni yenu kuhusu jinsi Kanuni za Camden zinatumika-tafadhali tuma maoni ama idhinisho lako kwa endorse@article19.org, na jina lako, unakotoka au shirika unalowakilisha na maoni.

Kazi hii imetolewa chini ya Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Leseni ya ShareAlike 2.5.

Uko huru kunakili, kusambaza na kuonyesha kazi hii na kuunda kazi zingine kutoka kwake, mradi;
1) Utambue ARTICLE 19;
2) Usitumie kazi hii kwa madhumuni ya kibiashara
3) Usisambaze kazi zozote zilizotolewa kwa chapisho hili chini ya leseni sawa na hii.

Kupata maelezo kamili ya kisheria ya leseni hii, tafadhali angalia: http://creative commons.org/licenses/by-nc-sa/2.5/legalcode

Utangulizi

Kanuni hizi zilitayarishwa na ARTICLE 19 kufuatia majadiliano yaliyohusisha kundi la maafisa wa ngazi za juu wa Umoja wa Mataifa na maafisa wengine, mashirika ya kiraia na wataalam wa masuala ya kitaaluma, katika sheria ya kimataifa ya haki za binadamu kuhusu masuala ya uhuru wa kujieleza na usawa katika mikutano iliyofanyika London 11 Desemba 2008 na 23-24 Februari 2009. Kanuni hizo zinawakilisha ufafanuzi wa kuendelea wa sheria ya kimataifa na viwango, desturi za Serikali zinazokubalika (kama inavyoonekana, miongoni mwa zingine, katika sheria za kitaifa na uamuzi wa mahakama za kitaifa) na kanuni za jumla za sheria zinazotambuliwa na jamii za mataifa.

Uundaji wa Kanuni hizi ulifuatia hamu ya kuimarisha zaidi uwiano wa utandawazi kuhusu uhusiano kati ya kuheshimu uhuru wa kujieleza na uimarishaji wa usawa. Ingawaje mgongano huenda ukaibuka kati ya dhamira za haki hizi zinazoshindana, mtazamo ulimwenguni umekuwa zaidi kwa uwezekano wa kuwepo kwa migongano hii badala ya suala muhimu la uhusiano mwema kati yao. Zaidi ya hayo, sheria ya kimataifa inatoa msingi wa kutatua migongano, kama iliyoelezewa katika Kanuni hizi.

Tunawaomba watu binafsi na mashirika kote ulimwenguni kuidhinisha Kanuni hizi kwa lengo la kuzipatia mamlaka na kuziunga mkono. Pia tunawaomba wanaofanya maamuzi, pamoja na watetezi, kuchukua hatua za kuanza kutekeleza Kanuni hizi katika ngazi zote.

Utangulizi

Kanuni hizi zimeundwa kwa ufahamu kuwa uhuru wa kujieleza na usawa ni haki za kimsingi, ambapo kufaulu kwake ni muhimu katika kufurahia na kulinda haki za binadamu. Pia husaidia kuunga na kupatia nguvu haki za binadamu.Hatua inayoratibiwa na yenye mwelekeo inapochukuliwa kuimarisha uhuru wa kujieleza na usawa, ndio mojawapo inaweza kutambuliwa vyema.

Ushirikishaji sekta mbalimbali na ujumuishaji kila upande ni vitambulisho vya uhuru wa kujieleza. Kupatikana kwa haki ya uhuru wa kujieleza huwezesha mjadala unaosisimua, wenye sura nyingi, maoni tofauti ya umma na kutoa sauti, mitazamo na maoni tofauti. Ukosefu wa usawa husababisha baadhi ya sauti kuwachwa nje, hali inayorudisha nyuma suala hili. Haki ya kila mmoja kusikizwa, kuongea na kushiriki katika siasa, sanaa na maisha ya kijamii ni muhimu, kwa upatikanaji na ufurahiaji wa usawa. Watu wanaponyimwa nafasi ya kushiriki na kutoa sauti kwa umma, masuala yao, tajriba na hofu zao huwa hazionekani, na wanakuwa katika hatari zaidi ya ulokole, kubaguliwa na kutengwa.

Mara nyingi, haki za uhuru wa kujieleza na usawa zimechukuliwa kama zinazotofautiana, ama kuhitilafiana moja kwa moja, huku mkazo ukitiliwa zaidi kwa mgongano baina yake. Kanuni zinatetea uhusiano wa kweli kati ya uhuru wa kujieleza na usawa, kutambua mchango wa kukamilishana na umuhimu inazotoa katika kuhifadhi na kulinda hadhi ya binadamu, na ukweli kuwa kuwepo pamoja ni muhimu kwa kutogawanya na kueneza kote haki za binadamu. Zikizingatiwa na kutiliwa maanani, zitawezesha haki za binadamu kwa wote ziheshimiwe.

Kanuni hizi pia zinatetea kuwa kuheshimu uhuru wa kujieleza na usawa kuna jukumu muhimu la kuchangia katika kuhakikisha demokrasia na ustawi wa kudumu wa binadamu, na kuimarisha amani ya kimataifa na usalama.
Hatua za usalama, hasa katika maeneo ya kukabiliana na ugaidi na uhamiaji, zimetatiza haki za kibinafsi, na kusababisha vikwazo haramu kwa uhuru wa kujieleza na unyanyapaa dhidi ya makundi fulani ya kikabila na kidini. Kanuni zinapinga wazo kuwa usalama unahitaji udhalimu wa haki za binadamu. Badala yake, zinatetea kuwa haki za binadamu ni msingi katika kupata usalama wa kweli.

Kanuni zinaelezea majukumu ya Serikali kuchukua hatua zinazofaa kuhimiza ushirikishaji sekta mbalimbali na ujumuishaji kila upande, kuimarisha upatikanaji sawa wa njia za mawasiliano, na kuhakikisha haki ya kupata habari.

Zinatetea jukumu jema la Nchi katika kuunda mazingira yanayofaa kwa uhuru wa kujieleza na usawa, huku ikitambua uwezekano wa dhuluma kutokea kwa sababu hiyo. Miundo dhabiti ya kidemokrasia- ambao ni pamoja na uchaguzi huru na wenye usawa, idara huru ya mahakama na mashirika ya kiraia yaliyosisimka- yanahitajika kuzuia utumizi mbaya na kufaulisha zaidi malengo ya ushirikishaji sekta mbalimbali na uwezo sawa. Ingawaje Nchi ina jukumu muhimu la kuchangia, udhibiti wa kibinafsi, pale inapofaa bado ndio bora zaidi kushughulikia masuala ya kitaalam yanayohusiana na vyombo vya habari.

Kanuni zinatambua umuhimu wa vyombo vya habari na njia zingine za mawasiliano ya umma katika kuwezesha uhuru wa kujieleza na katika kuwezesha usawa, kwa kuhakikisha uwezo sawa. Vyombo vya habari vya kitamaduni vinaendelea kuchangia jukumu muhimu kote ulimwenguni, ingawaje vinapitia mabadiliko makubwa. Teknolojia mpya- ambazo ni pamoja na utangazaji wa njia ya mtandao, simu za

rununu na Mtandao- zimeimarisha pakubwa usambazaji wa habari na kufungua aina mpya za mawasiliano, kama tovuti tofauti. Wakati huo huo, katika sekta nyingi za vyombo vya habari, uwezo wa kufikia vyombo vya habari hasa makundi ya wachache, na ujumuishaji wa dhati wa kila upande katika vyombo vya habari unatishwa na ongezeko la umiliki wa vyombo vya habari na changamoto zingine za soko, pamoja na soko kutofaulu.

Mabadiliko haya yanaleta nafasi na pia changamoto kwa ushirikishaji sekta na yanayohusu umma. Sera zinazofaa na mifumo ya udhibiti inayolinda ushirikishaji sekta mbalimbali na ujumuishaji kila upande inahitajika, lakini lazima ijumuishwe katika mazungumzo ya kina ya kijamii yanayovutia mjadala mpya kuhusu jukumu la vyombo vya habari katika jamii na kuhusisha washikadau kutoka jamii tofauti pamoja na waakilishi wa vyombo vya habari, wakuu wa umma, serikali na mashirika ya kiraia.

Kanuni hizi zinaegemea pakubwa kwa fikra za usawa, ambazo zinajumuisha haki ya usawa mbele ya sheria na kutobaguliwa, pamoja na wazo la hali na kushughulikiwa kwa usawa. Zinatambua kwamba matatizo ya ubaguzi na fikra mbaya ni masuala yaliyokita mizizi katika jamii na uchumi na pia kisiasa. Kuondolewa kwake kunahitaji juhudi nyingi za kudumu, ambazo ni pamoja na katika masuala ya elimu, mazungumzo ya kijamii na uhamasishaji. Kukagua mijadala kuhusu masuala yenye utata, ambayo ni pamoja na dini, hakutasuluhisha sababu zilizopo za chuki inayotatiza usawa. Kwa hali nyingi, vikwazo kwa uhuru wa kujieleza hulenga makundi yasiyobahatika, kutatiza badala ya kuimarisha usawa. Mjadala wa wazi ni bora kuliko vikwazo katika kukabiliana na fikra mbaya za watu binafsi na makundi na kuweka wazi madhara yanayochangiwa na chuki.

Kanuni hata hivyo, zinatambua kuwa aina fulani ya matamshi, kwa mfano kuchochea chuki ya kimbari kwa kusudi, ni hatari kwa usawa na inastahili kukatazwa. Masharti yanayokataza matamshi ya aina hiyo yanastahili kufafanuliwa kwa upana ili kuzuia utumizi mbaya wa vikwazo, ambao ni pamoja na sababu za kisiasa. Hatua mwafaka zinastahili kuchukuliwa kuhakikisha kuwa masharti hayo yanatumika kwa usawa kwa manufaa ya makundi yote yanayolindwa. Kwa sababu hii, hatua ya kufuata kesi baada ya kesi ambayo inaangalia hali na uwezo wa madhara ni muhimu, hasa kwa upande wa wakuu wa mahakama. Masharti ya aina hiyo yanastahili kutumika kulinda watu binafsi na makundi pekee. Hayafai kuchochewa kulinda imani fulani, misimamo ama dini.

Mwisho, Kanuni zinatambua kwamba uhuru wa kujieleza na usawa unahimiza ukuaji na uchangamfu wa mashirika ya kiraia ambayo hatimaye hutoa sauti na kuyatambua makundi yasiyobahatika pamoja na kujitahidi kulinda haki zao. Kanuni hizi pia zinatetea kwa dhati dhamira iliyoelezwa katika Utangulizi wa Azimio la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu kwamba kila mtu binafsi na kitengo cha jamii kitajitahidi kuimarisha heshima kwa uhuru wa kujieleza na usawa na kulinda utambulizi wao kila mahali.

Sisi, watu binafsi na mashirika, [1]tunaidhinisha Kanuni hizi na kupendekeza kuwa mashirika husika katika ngazi za kitaifa, maeneo na kimataifa zichukue hatua za kuimarisha usambazaji wake, ufahamu, kukubalika na utekelezaji wake.

[1]Orodha kamili ya wale walioidhinisha kanuni hizi ipo katika tuvuti ya ARTICLE 19, www.article19.org

Kanuni

1.Sheria zinazolinda usawa na uhuru wa kujieleza

Kanuni 1: Uidhinishaji na ujumuishaji wa sheria ya haki za binadamu

Nchi zote zinastahili kuidhinisha na kuangazia katika sheria zake za nyumbani, kupitia ushirikishaji ama njia nyingine, mikataba ya kimataifa na maeneo ya haki za binadamu zinazohakikisha haki za usawa na uhuru wa kujieleza.

Kanuni 2: Mfumo wa Sheria unaolinda haki ya uhuru wa kujieleza

2.1. Nchi zinastahili kuhakikisha kuwa haki ya uhuru wa maoni na kujieleza, kupitia kwa njia ya mawasiliano, ambayo ni pamoja na haki ya habari, inawekwa katika yaliyomo kwa katiba ya nyumbani ama sawa na hiyo, kulingana na sheria za kimataifa za haki za binadamu.

2.2. Hususan, Nchi zinastahili kuhakikisha vitengo vya kikatiba vinaeleza wazi malengo ya vikwazo vinavyokubalika kwa haki ya uhuru wa kujieleza, na kujumuisha kuwa vikwazo vya aina hiyo vinakubalika kisheria, kufafanuliwa kwa upana kuhudumia haja halali inayotambulika katika katiba, na kuwa na umuhimu katika jamii ya kidemokrasia kulinda haja hiyo.

2.3. Nchi zinastahili kuanzisha mfumo wazi wa sheria za kulinda haki ya habari, ambayo ni pamoja na haki ya kufikia habari inayoshikiliwa na mashirika ya umma, na kuimarisha ufichuzi wa habari.

Kanuni 3: Mfumo wa sheria unaolinda haki ya usawa

3.1. Nchi zinastahili kuhakikisha haki ya usawa inajumuishwa katika maelezo ya kikatiba ya nchi ama sawa na hayo, kulingana na sheria ya kimataifa ya haki za binadamu.

3.2. Sheria ya nchi husika lazima ihakikishe kuwa:

i. Watu wote wako sawa mbele ya sheria na wana haki ya ulinzi sawa wa kisheria.

ii. Kila mtu ana haki ya kuwa huru dhidi ya ubaguzi wowote haswa ule unafatilia mbari, ulemavu, rika,hali ya kinjinsia, lugha, siasa ama maoni mengine, taifa asili ama anakotoka kijamii, mali ya kuzaliwa ama hali nyingine.

3.3. Nchi zinastahili kuanzisha mfumo wa wazi wa kisheria na sera ya kukabiliana na hali tofauti za ubaguzi, ambazo ni pamoja na uhangaishaji, na kwa kutambua haki ya usawa, ambayo ni pamoja na uhuru wa kujieleza.

Kanuni 4: Kupata Suluhisho

4.1. Nchi zinastahili kuhakikisha upatikanaji wa uwezo na suluhisho zinazofaa za ukiukaji wa haki za binadamu, ambazo ni pamoja na ukiukaji wa haki za uhuru wa kujieleza na usawa. Haya yanastahili kujumuisha suluhisho za mahakama na zisizo za mahakama, kama ilivyokuwa kabla ya taasisi za haki za binadamu na/ama ofisi ya malalamishi ya umma.

4.2. Nchi zinastahili kuhakikisha kuwa haki ya kusikizwa hadharani na kwa usawa na jopo lililohitimu, lililo huru na bila mapendeleo na lililobuniwa kisheria inahakikishwa.

II. Haki ya kusikizwa na haki ya kuzungumza

Kanuni 5: Mfumo wa Sera ya Umma ya ushirikishaji sekta mbali mbali na usawa

5.1. Nchi zote zinastahili kuwa na sera ya umma na mfumo wa udhibiti kwa vyombo vya habari, pamoja na vyombo vipya vya habari, ambavyo vinaimarisha ushirikishaji sekta mbalimbali na usawa, kulingana na yafuatayo:

i. Mfumo unastahili kuheshimu kanuni muhimu kwamba udhibiti wowote wa vyombo vya habari unastahili kuendeshwa na mashirika huru kutoka kwa serikali, ambayo yanawajibika hadharani na yanayoendeshwa wazi.

ii. Mfumo unastahili kuimarisha haki za jamii tofauti kufikia na kutumia kwa njia huru vyombo vya habari na teknolojia za habari na mawasiliano kwa utayarishaji na usambazaji wa maelezo yao wenyewe, pamoja na kupokewa kwa maelezo yaliyotayarishwa na wengine, bila kujali wanaoyatoa.

5.2. Mfumo huu unastahili kutekelezwa miongoni ya mengine, kupitia hatua zifuatazo:

i. Kuimarisha uwezo wa kufikia wote na wenye gharama nafuu kwa njia za mawasiliano na upokezi wa huduma za vyombo vya habari, ambazo ni pamoja na simu, Mtandao na umeme.

ii. Kuhakikisha kuwa hakuna ubaguzi katika haki ya kuanzisha magazeti, redio na televisheni, na mifumo mingine ya mawasiliano.

iii. Kutenga nafasi ya 'kutosha' kwa matumizi ya utangazaji kwa mbinu tofauti za mawasiliano kuhakikisha kuwa, kwa jumla, umma unaweza kupokea huduma tofauti za utangazaji.

iv. Kutenga rasilmali sawa, ambazo ni pamoja na masafa, miongoni mwa huduma za umma, vyombo vya habari vya kibiashara na kijamii, ili wote waweze kuwakilisha tamaduni tofauti, jamii na maoni katika jamii.

v. Kuhitaji mashirika yanayosimamia vidhibiti vya vyombo vya habari kuangazia pakubwa jamii kwa ujumla.

vi. Kuweka hatua zinazofaa kuzuia umilikaji usiostahili wa vyombo vya habari.

vii. Kutoa usaidizi kwa umma, uwe wa kifedha ama aina nyingine, kupitia njia huru na wazi, na kulingana na mpangilio wenye malengo, kuimarisha kuwepo kwa habari za kutegemewa, zinazoshirikisha wote na wakati unaofaa kwa wote, na utayarishaji wa maelezo ambayo hutoa mchango muhimu kwa ujumuishaji tofauti na unaoimarisha mazungumzo miongoni mwa jamii tofauti.

5.3. Mfumo huu unastahili pia kujumuisha hatua zifuatazo:

i. Kupinga vikwazo vyovyote kwa utumizi wa lugha za wachache ambavyo vina athari

ya kuvunja moyo ama kuzuia vyombo vya habari vinavyoshughulikia hasa jamii tofauti.

ii. Kuunda ujumuishaji, ambao ni pamoja na vyombo vya habari vinavyolenga jamii tofauti, moja wapo ya mbinu za kukagua maombi ya leseni za utangazaji.

iii. Kuhakikisha makundi yasiyobahatika na yaliyobaguliwa yana uwezo sawa wa kufikia rasilmali za vyombo vya habari, ambazo ni pamoja na nafasi za mafunzo.

5.4. Maadili ya huduma za umma katika vyombo vya habari yanastahili kulindwa na kuhimizwa kwa kubadilisha mifumo ya vyombo vya habari vinavyosimamiwa na Nchi ama serikali, kwa kupatia nguvu mitandao ya utangazaji ya huduma za umma iliyopo, na kuhakikisha ufadhili wa kutosha kwa vyombo vya habari vya huduma za umma, kuhakikisha ushirikishaji, uhuru wa kujieleza na usawa katika muundo wa vyombo vya habari unaobadilika.

Kanuni 6: Jukumu la Vyombo vyote vya habari

6.1 Vyombo vyote vya habari vinastahili, kama wajibu wa kitabia na kijamii, kuchukua hatua za:

i. Kuhakikisha wafanyakazi wake ni tofauti na wanawakilisha jamii kwa ujumla.

ii. Kushughulikia jinsi iwezekanavyo hofu za makundi yote katika jamii.

iii. Kutafuta duru za aina tofauti na sauti miongoni mwa jamii tofauti, badala ya kuwasilisha jamii kama makundi ya kipekee.

iv. Kufuata viwango vya hali ya juu vya utoaji habari ambavyo vinafikia viwango vinavyotambulika vya kitaalam na kimaadili.

Kanuni 7: Haki ya Kurekebisha na Kujibu

7.1. Haki za kurekebisha na kujibu zinastahili kuhakikishwa kulinda haki ya usawa na kutobaguliwa, na usambazaji huru wa habari.

7.2. Utekelezaji wa haki ya kurekebisha na kujibu haufai kuzuia suluhisho zingine, ingawaje huenda ukafikiriwa wakati wa kuangalia suluhisho zingine, kwa mfano kupunguza malipo ya madhara.

7.3. Haki hizi zinalindwa vyema kupitia kwa mifumo ya kujidhibiti wenyewe. Hakuna haki ya lazima ya kujibu ama kurekebisha inastahili kuwekwa ikiwa mfumo wa kujidhibiti wenyewe upo.

7.4. Haki ya marekebisho humpatia mtu yeyote haki ya kutaka kuona vyombo vya habari vinachapisha ama kutangaza marekebisho ikiwa chombo hicho cha habari kimewahi kuchapisha ama kutangaza habari zenye makosa.

7.5. Haki ya kujibu humpatia mtu yeyote haki ya kufanya chombo cha habari kisambaze jibu lake ikiwa chapisho ama tangazo lililotolewa na chombo hicho

III. Kuhimiza utangamano baina ya watu wa tamaduni tofauti

cha habari halina maelezo ya sawa ama ni ya kupotosha na yameingilia haki inayotambulika ya mtu huyo, na ambapo urekebishaji hauwezi kutarajiwa kutatua kosa.

Kanuni 8: Majukumu ya Nchi

8.1. Nchi zinastahili kuwapatia majukumu maafisa wa umma katika ngazi zote, pamoja na mawaziri, kuzuia kutoa taarifa zinazochochea ubaguzi ama kuzuia usawa na maelewano kati ya watu wa tamaduni tofauti. Kwa watumishi wa umma, haya yanastahili kuonyeshwa katika maadili rasmi ya tabia ama masharti ya kuajiriwa.

8.2. Nchi zinastahili kuhusika na juhudi kubwa za kukabiliana na fikra mbaya za, na ubaguzi dhidi ya, watu binafsi na makundi na kuimarisha ufahamu wa tamaduni tofauti na tathmini, ambazo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu kuhusu thamani za haki za binadamu na kanuni na kwa kufahamisha ama kupatia nguvu ufahamu wa tamaduni tofauti kama sehemu ya mtaala wa shule kwa wanafunzi wa umri wote.

Kanuni 9: Majukumu ya vyombo vya habari

9.1. Vyombo vyote vya habari vinastahili kama jukumu la kitabia na kijamii, kuchangia wajibu wa kukabiliana na ubaguzi na kuimarisha ufahamu wa tamaduni tofauti, pamoja na kutafakari yafuatayo:

i. Kuzingatia kuripoti jinsi hali ilivyo na kwa njia ya kweli na yenye kujali, huku ikihakikisha kwamba umma unafahamishwa kuhusu vitendo vya ubaguzi.

ii. Kuwa macho kwa hatari ya ubaguzi ama fikra mbaya za watu binafsi na makundi yanayoendelezwa na vyombo vya habari.

iii. Kuzuia kuzungumzia bila sababu, mbari, dini, jinsia na maelezo mengine ya kundi ambayo huenda yakasababisha ukosefu wa uvumilivu.

iv. Kuhamasisha kuhusu madhara yanayosababishwa na ubaguzi na fikra mbaya.

v. Kuripoti kuhusu makundi tofauti ama jamii na kuwapatia wanachama wao nafasi ya kuzungumza na kusikizwa kwa njia inayohimiza njia bora ya kuwaelewa, na wakati huo huo, kuangazia mtazamo wa makundi hayo ama jamii.

9.2. Watangazaji wa huduma za umma wanastahili kuwa na wajibu wa kuzuia fikra mbaya za watu binafsi na makundi, na jukumu lao linastahili kuwahitaji kuimarisha ufahamu wa tamaduni tofauti na kuendeleza ufahamu wa jamii tofauti na masuala wanayokabiliwa nayo. Hii inastahili kujumuisha upeperushaji wa vipindi vinavyoonyesha jamii tofauti kama wahusika sawa katika jamii.

9.3. Maadili ya kitaalam ya tabia kwa vyombo vya habari na wanahabari yanastahili kuangazia kanuni za usawa na njia zinazofaa zinastahili kuchukuliwa kutangaza rasmi na kutekeleza maadili hayo.

9.4. Vipindi vya kitaalam vya maendeleo kwa wataalam wa vyombo vya habari vinastahili kuhamasisha kuhusu jukumu ambalo vyombo vya habari vinaweza kuchangia katika kuimarisha usawa na haja ya kuzuia fikra mbaya.

Kanuni 10: Wahusika wengine

10.1 Wanasiasa na watu wengine waliopo uongozini katika jamii wanastahili kuzuia kutoa taarifa ambazo huenda zikahimiza ubaguzi ama kudhuru usawa, na wanastahili kutumia nafasi zao kuimarisha ufahamu wa tamaduni tofauti, ambazo ni pamoja na kupinga, panapostahili, taarifa za ubaguzi ama tabia.

10.2. Mashirika ya kiraia yanastahili kuheshimu mfumo unaotambua maoni tofauti, na kuimarisha haki za uhuru wa kujieleza na usawa kulingana na Kanuni hizi. Hasa, wanastahili kuimairisha ufahamu wa tamaduni tofauti, kukubali sauti tofauti, na kuunga uwezo wa watu wa jamii tofauti, na hasa makundi ya wachache, kutoa maoni na hofu zao, kwa njia ambayo inatambua ujumuishaji wa ndani katika jamii.

IV.Uhuru wa kujieleza na taarifa zenye madhara

Kanuni 11:Vikwazo

11.1. Nchi hazifai kuweka vikwazo vyovyote kwa uhuru wa kujieleza ambavyo havilingani na viwango vilivyoelezwa katika Kanuni 2.2 na, hasa, vikwazo vinastahili kutolewa na sheria, kutumika kulinda haki na heshima za wengine, usalama wa kitaifa ama mpangilio wa umma, ama afya ya umma ama tabia, na viwe vinastahili katika jamii yenye demokrasia kulinda masuala haya. [2]Hii inamaanisha, miongoni ya mambo mengine, kuwa vikwazo:

i. Vimefafanuliwa wazi na kwa upana na vinashughulikia haja ya lazima katika jamii.

ii. Ndio hatua zilizopo ambazo haziingilii sana, kwa fikra kuwa hakuna hatua nyingine ambayo itafaa na pia kuzuia uhuru wa kujieleza.

iii. Hazijafafanuliwa sana, kwa maana kuwa hazizuii taarifa kwa njia kubwa ama ambayo haijalengwa, ama zinapita maelezo ya taarifa mbaya na kupuuza taarifa halali.

iv. Zinalingana kwa fikra kuwa manufaa kwa kinacholindwa kinazidi madhara kwa uhuru wa kujieleza, ambazo ni pamoja na vikwazo wanavyoidhisha.

11.2 Nchi zinastahili kuangalia upya mfumo wao wa kisheria kuhakikisha kuwa vikwazo vyovyote kwa uhuru wa kujieleza vinalingana na yaliyoelezwa juu.

[2]Hii ni kulingana na Kifungu cha 19 (3) cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa

Kanuni 12: Kuchochea Chuki

12.1. Nchi zote zinastahili kuchukua sheria zinazozuia utetezi wowote wa chuki za kitaifa, kimbari ama dini ambazo zinahusisha uchochezi ama ubaguzi, uadui ama ghasia (matamshi/taarifa ya chuki).[3] Mifumo ya kisheria ya kitaifa inastahili kueleza wazi, kwa kusema ukweli ama kupitia kwa ufafanuzi wa mamlaka, kuwa:

i. Maneno 'chuki' na 'uhasama' yanahusisha hisia kali na zisizo na sababu zinazosababisha aibu, uadui na chuki dhidi ya kundi linalolengwa.

ii. Neno 'utetezi' linastahili kueleweka kama linalohitaji nia ya kuimarisha chuki hadharani dhidi ya kundi linalolengwa.

iii. Neno 'uchochezi' linahusisha taarifa kuhusu makundi ya kitaifa, kimbari ama kidini ambayo yanachangia hatari ya ubaguzi, uhasama ama ghasia dhidi ya watu wanaohusika na makundi hayo.

iv. Uimarishaji wa utambulizi unaofaa na jamii tofauti, hauchangii taarifa za chuki.

12.2 Nchi zinastahili kuzuia upuuzaji ama ukanushaji wa uhalifu wa mauaji ya halaiki, makosa dhidi ya ubinadamu na makosa ya kivita, isipokuwa wakati ambapo taarifa hizo zinahusisha matamshi ya chuki kama ilivyofafanuliwa na Kanuni 12.1.

12.3. Nchi zinastahili kuzuia ukosoaji uliolekezwa kwa, ama mjadala kuhusu, maoni fulani, imani na misimamo, ama dini ama taasisi za kidini, isipokuwa kama maelezo hayo yanahusisha taarifa za chuki kama ilivyofafanuliwa na Kanuni 12.1.

12.4. Nchi zinastahili kuhakikisha kuwa watu ambao wamepata madhara ya kweli kwa sababu ya taarifa za chuki kama ilivyofafanuliwa na Kanuni 12.1 wana haki ya suluhisho linalofaa, ambalo ni pamoja na suluhisho la kiraia kwa madhara.

12.5. Nchi zinastahili kuangalia upya mfumo wao wa kisheria kuhakikisha kuwa kanuni zozote za taarifa za chuki zinakubaliana na yaliyopo juu.

[3]Hii ni kulingana na Kifungu cha 20 (2) cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa.

Appendix A

Wataalam wafuatao (waliopangwa kwa alfabeti) walishiriki kwa uwezo wao wa kibinafsi katika mashauriano ambayo yalitayarisha Kanuni hizi. Mashirika na walioshirikishwa wameorodheshwa kwa madhumuni ya utambulizi pekee. Kuorodheshwa kwao hakupendekezi idhinisho rasmi la Kanuni.

Eva Smith Asmussen, Mwenyekiti, European Commission against Racism and Intolerance, Strasbourg, Ufaransa

Hossam Bahgat, Mkurugenzi, Egyptian Initiative for Personal Rights, Cairo, Misri

Kevin Boyle, Profesa wa Sheria, Chuo Kikuu cha Essex, Colchester, Uingereza

Barbora Bukovsk`a, Mkurugenzi wa ngazi za juu wa Sheria, ARTICLE 19, London, Uingereza

Sandra Coliver, Afisa wa Sheria wa Ngazi za Juu, Open Society Justice Initiative, New York, Amerika

Anastasia Cricklely, Mwenyekiti, shirika la EU Fundamental Rights Agency, Vienna, Austria

Cece Fadope, Afisa wa Mipango wa Afrika, ARTICLE 19, London, Uingereza

Bambang Harymurti, Mhariri, Jarida la Tempo, Jakarta, Indonesia

Pierre Hazan, Mshauri, Ofisi ya Mwakilishi wa Haki za Binadamu, Geneva, Uswizi

Sa'eda Kilani, Mkurugenzi, Arab Archives Institute, Amman, Jordan

Mark Lattimer, Mkurugenzi, Minority Rights Group International, London, Uingereza

Toby Mendel, Wakili wa Kisheria wa Ngazi za Juu, ARTICLE 19, London, Uingereza

Githu Muigai, Mjumbe Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu aina za kisasa za ubaguzi wa kimbari, utenganisho wa kimbari, ubaguzi wa uraia na mambo yanayohusiana na kutovumiliana, Nairobi, Kenya

Mario Oetheimer, Wakili, European Court of Human Rights, Strasbourg, Ufaransa

Sejal Parmar, Wakili wa Ngazi za Juu, ARTICLE 19, London, Uingereza

Borisilave Petranov, Mkurugenzi wa Mipango ya Haki za Kiraia na Kisiasa na Naibu Mkurugenzi wa Sigrid Rausing Trust, London, Uingereza

Dimitrina Petrova, Mkurugenzi Mkuu , Equal Rights Trust, London, Uingereza

Malak Poppovic, Mkurugenzi Mkuu, Conectas Human Rights, London, Sao Paolo, Brazil

Dubravka (s)imonovic, Mwanachama, Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Kumaliza Ubaguzi Dhidi ya Wanawake , Zagreb, Croatia

Michael Wiener, Ofisa wa Haki za Binadamu, Ofisi ya Mwakilishi wa Kitengo cha Utaratibu Maalum wa Haki za Binadamu, Geneva, Uswizi

Aidan White, Katibu Mkuu, International Federation of Journalists, Brussels, Ubelgiji

ARTICLE 19

GLOBAL CAMPAIGN FOR FREE EXPRESSION

Kanuni za Camden kuhusu Uhuru wa Kujieleza na Usawa zimeundwa kwa ufahamu kuwa ni haki za msingi. Uhuru wa kujieleza na usawa ni haki muhimu zinazochangia jukumu muhimu la kulinda hadhi ya binadamu, kuhakikisha demokrasia na kuhimiza amani ya kimataifa na usalama.

Kanuni za Camden zinawakilisha ufafanuzi wa kuendelea mbele wa sheria ya kimataifa na viwango, desturi za serikali zilizokubalika na kanuni za jumla za sheria zinazotambuliwa na jamii ya mataifa. Kanuni hizi zilitayarishwa na ARTICLE 19, kwa mashauriano na maafisa wa ngazi za juu wa Umoja wa Mataifa pamoja na maafisa wengine, mashirika ya kiraia na wataalam wa kitaaluma. Stakabadhi hii iliundwa kuhimiza uwiano zaidi wa utandawazi kuhusu uhusiano kati ya kuheshimu uhuru wa kujieleza na uimarishaji usawa.